



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na:SDC/S.10/45A /55

Tarehe: 04.05.2023.

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI IMEPOKEA KIBALI CHA AJIRA KUMB.NA. FA.97/228/01 "TEMP"/06 CHA TAREHE 06/04/2023 KUTOKA KWA KATIBU MKUU, OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA. KIBALI HICHO KIMETOA IDHINI YA KUAJIRI NAFASI ZA WATENDAJI WA VIJIJI NA WAANDISHI WAENDESHA OFISI (MAKATIBU MUHTASI).

KUTOKANA NA KIBALI HICHO HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI INATANGAZA NAFASI ZA KAZI ZIFUATAZO:-

1.MTENDAJI WA KIJIKI DARAJA LA III - NAFASI KUMI NA MOJA (11).

(a) SIFA ZA MWOMBAJI:-

Awe mwenye Elimu ya kidato cha Nne (IV) au kidato cha sita (VI), aliyehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika moja ya fani zifuatazo:- Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Usimamizi wa Fedha, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Jamii kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

(b) Mshahara kwa kuzingatia Ngazi ya Mishahara ya Serikali yaani TGS B.1 kwa Mwezi.

(c) KAZI NA MAJUKUMU YA MTENDAJI WA KIJIKI:-

- i. Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiki.
- ii. Kusimamia Ulinzi na Usalama wa Raia na Mali zao, kuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiki.
- iii. Kuratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo
- iv. Katibu wa Mikutano na Kamati zote za Halmashauri ya Kijiki.
- v. Kutafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu.
- vi. Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- vii. Kiongozi wa Wakuu wa Vitengo vya Kitaalam katika Kijiki.
- viii. Kusimamia Kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na Nyaraka za Kijiki.
- ix. Mwenyekiti wa kikao cha Wataalam waliopo katika Kijiki.
- x. Kupokea, kusikiliza na kutatua migogoro ya wananchi.
- xi. Kusimamia utungaji wa sheria ndogo za Kijiki na
- xii. Atawajibika kwa Mtendaji wa Kata.

2. WAANDISHI WAENDESHA OFISI (PERSONAL SECRETARY III) NAFASI TATU (03).

(a) SIFA ZA MWOMBAJI:-

- Awe amehitimu Kidato cha nne au Sita, aliyehudhuria mafunzo ya uhaziri na kufaulu mtihani wa Hatua ya Tatu.
- Awe amepata mafunzo ya Kompyuta kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali na kupata cheti katika program za Windows, Microsoft Office, Internet, E-mail na Publisher.

(b) KAZI NA MAJUKUMU YA WAANDISHI WAENDESHA OFISI DARAJA III.

- i. Kuchapa barua, Taarifa na nyaraka za kawaida.
- ii. Kusaidia kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza sehemu wanapoweza kushughulikiwa.
- iii. Kusaidia kutunza Taarifa/kumbukumbu za matukio, miadi, wageni, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba ya kazi zingine zilizopangwa kutekelezwa katika Ofisi anayofanya kazi na kumtaarifu Mkuu wake kwa wakati unaohitajika.
- iv. Kusaidia kutafuta na kumpatia Mkuu wake wa kazi kwa wasaidizi wake na pia kumuarifu kuhusu Taarifa zozote anazokuwa amepewa na wasaidizi hao.
- v. Kusaidia kupokea majalada, kuyagawa kwa Maofisa walio katika sehemu alipo, na kuyakusanya, kuyatunza na kuyarudisha sehemu zinazohusika.
- vi. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na msimamizi wake wa kazi.
- vii. ***Mshahara kwa kuzingatia Ngazi ya Mishahara ya Serikali yaani TGS.B/1 kwa mwezi.***


MASHARTI YA JUMLA:-

- i. Waombaji wote wawe na umri kati ya miaka 18 hadi 45
- ii. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania
- iii. Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (CV) yenye Anuani na namba za simu na majina mawili ya wadhamini.
- iv. Waombaji wote wawe na kitambulisho cha NIDA au namba za kitambulisho.
- v. Waombaji wote waambatanishe picha mbili za "Passport size" za hivi karibuni na ziandikwe jina kwa nyuma.
- vi. Watakaofaulu kuitwa kwenye usaili majina au orodha yao itawekwa kwenye tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti ambayo ni www.serengetidc.go.tz.
- vii. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **19.05.2023 saa 09:30** Alasiri.

MAOMBI YOTE YATUMWE KWA:-

MKURUGENZI MTENDAJI (W),
S.L.P.176,
MUGUMU/SERENGETI.

**Imetolewa Leo,
Tarehe 04.05.2023 na:-**



Kivuma H. Msangi
Mkurugenzi Mtendaji (W)
SERENGETI.

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI
S. L. P 176
MUGUMU / SERENGETI